JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.
OFISI YA RAIS – TAMISEMI.
HALMASHAURI YA MJI MAFINGA.

NAMBA ZA SIMU:
MKUU WA SHULE 0768056996

M/MKUU WA SHULE 0624174277
OFISI YA MALEZI 0762-186-070
0712645589

SHULE YA SEKONDARI J. JMUNGAI,
S.L.P 226,
MAFINGA.

TAREHE: …….

NDUGU MZAZI / MLEZI WA MWANAFUNZI……
S.L.P …….
……...

YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI J.J. MUNGAI MWAKA 2022/2023

1. Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2022 tahasusi ya **……...** Muhula wa masomo unaanza tarehe **……** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **……...** Bila kuchelewa na mwisho wa kuripoti ni tarehe **…….**

MAHALI SHULE ILIPO.

Shule ya sekondari J.J. Mungai ipo mkoani Iringa katika halmashauri ya Mji Mafinga, umbali wa 1.5 kilomita kutoka kituo kikuu cha mabasi Mafinga .Kutoka kituo cha mabasi Mafinga kuna usafiri wa taxi, nauli ni shilingi elfu tano tu (5,000) hadi shuleni

MUHIMU.

Hakikisha mwanafunzi anafanyiwa uchunguzi wa afya yake katika hospitali ya Wilaya au Mkoa na kujaziwa Fomu maalumu ya kupimwa afya **(FORM "A")** na Mganga Mkuu. Fomu imeambatanishwa. Pia hatapokelewa bila kutimiza maagizo muhimu kama yalivyoorodheshwa kwenye maelezo yanayofuata.

NIDHAMU NA TAALUMA.

Shule hii ina sifa nzuri kwa nidhamu na taaluma, mwanafunzi atatakiwa kufuata taratibu na sheria zote za shule awapo shuleni. Utovu wa nidhamu wa aina yoyote hautovumiliwa na kupelekea mwanafunzi kufukuzwa shule.

2. MAHITAJI MUHIMU YA SHULE.

1) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi elfu sabini tu (**70,000/=**) unaweza kutoa shilingi **35,000/=** kwa nusu mwaka na kiasi kilichobaki muhula wa pili.
2) Fedha ya tahadhari (Caution money) Sh. **5,000/=**
3) Mchango wa huduma ya kwanza shuleni Sh. **10,000/=**
4) Kitambulisho Sh. **6,000/=**
5) Mchango wa taaluma Sh. **20,000/=**
6) Mchango wa mlinzi, mpishi Sh. **30,000/=**
7) Mchango wa samani Sh. **17,000/=**
8) Mitihani ya kujipima (mock) Sh. **30,000/=**

Jumla.	**188,000/=**

✓ Mzazi atatakiwa kutoa kiasi cha shilingi 188,000/= kwa mwaka mzima au kiasi cha shilingi 153,000/= kwa nusu mhula ili mwanafunzi aweze kupokelewa shuleni

MUHIMU:

Michango yote inatakiwa ilipwe muhula wa kwanza ambayo gharama yake ni 153,000/=. Ada tu ndio inaruhusiwa kulipwa kwa awamu mbili, yaani 35000/= kwa muhula wa kwanza na 35,000 kwa muhula wa pili.

NAMNA YA KULIPA ADA NA MICHANGO MINGINE

A. Ada yaani **Sh. 70,000=** kwa mwaka au **35,000=** kwa nusu muhula ziwekwe kwenye Akaunti ya Shule **Namba 60201200062 yenye Jina J.J. Mungai Secondary School. NMB Bank Plc**

B. Michango mingine yote (ada haihusishwi) yaani kuanzia Namba 2-8 hapo juu iwekwe kwenye Akaunti **Namba 60202300234 yenye Jina J.J. Mungai Secondary School. NMB Plc**

ZINGATIA KUWA:

- ✓ PESA IKISHALIPWA HAIRUDISHWI KWA SABABU YEYOTE ILE
- ✓ FEDHA TASLIMU HAZITAPOKELEWA SHULENI.
- ✓ **Mwanafunzi anatakiwa aje na kadi ya Bima ya Afya kwa ajili ya matibabu yake, na kwa wale wasiokuwa na bima, mzazi atatakiwa kumwachia kiasi cha pesa mwanafunzi kwa ajili ya matibabu.**

MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI

i Ream ya karatasi 1 (kwa mwaka)
ii File 3 (spring file)
iii Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
iv Scientific calculator
v Godoro kwa wanafunzi (futi 2 ½) Dodoma TX cover

vi Blanket 1 la kawaida kwani mazingira ni ya baridi

vii Mashuka 2, 1 rangi ya pink na 1 rangi ya light blue

viii Tranka imara kwa ajili ya kuhifadhi vifaa vyake

ix Vifaa vya chakula na vyombo vingine: kontena, kikombe cha chai, kikombe cha kuogea, kijiko 1 na ndoo za plastiki 2.

KWA UPANDE WA MASOMO MWANAFUNZI AJE NA

i. Dafati kubwa (counter book quire 4) zisizopungua 10

ii. Daftari ndogo (msoni) zisizopungua 10

iii. Kalamu za kutosha

iv. Mkebe (mathematical set)

v. School bag ni lazima kwa ajili ya kubebea vifaa vya darasani

SARE ZA SHULE NA MALAZI.

(A) WASICHANA.

1. Sketi za rangi ya maroon mbili (siyo damu ya mzee) zenye marinda box na zilizo ndefu kufika chini, makoti mawili (ya kitambaa cha sketi) pamoja na tai ili kufanya suti,
2. Nguo za kushindia (shamba dress) gauni la blue (Esteem Material)
3. Tshirt ya bluu
4. Rangi ya hijabu kwa waislam tu (kijuba) iwe nyeupe na isiyo na urembo, rangi nyingine haziruhusiwi
5. Mashati meupe mikono mirefu mawili
6. Soksi nyeupe jozi mbili
7. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba na vyenye visigino vifupi.
8. Tracksut ya rangi bluu
9. Pull neck nyeusi
10. Jaketi jeusi liliso na maandishi wala kofia **(Maprova na majaketi marefu yanayovuka magoti hayaruhusiwi shuleni)**
11. Aje na raba nyeupe kwa ajili ya michezo jozi moja ambazo atazivaa muda wa michezo tu. Michezo kwetu ni taaluma hivyo ni lazima.

(B) WAVULANA.

1. Suruali mbili (2), makoti mawili rangi ya maroon, pamoja na tai
2. Nguo ya kushindia (shamba dress) yaani suruali ya blue ambayo itavaliwa na tshirt ya bluu (Esteem Material)

3.Tshirt rangi ya bluu
4.Mashati meupe mikono mirefu mawili
5.Soksi nyeupe jozi mbili
6.Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
7.Traksut yenye nembo ya shule rangi ya bluu
8.Pull neck nyeusi
9.Jaketi jeusi liliso na maandishi wala kofia (Maprova na majaketi marefu yanayovuka magoti hayaruhusiwi shuleni).
10. Aje na viatu vya michezo jozi moja ambavyo atavivaa muda wa michezo tu. Michezo kwetu ni taaluma hivyo ni lazima

ZINGATIA:

- ✓ Ili kuepuka kuchanganya rangi katika sare za shule, unashauriwa sare kushonea Mafinga kwani mafuundi wapo.
- ✓ Mavazi mengine tofauti na yale yaliyoelekezwa hayaruhusiwi kabisa, tofauti na hapa sheria za shule zitachukua nafasi yake. Ukaguzi utafanyika ili kuhakiki vifaa alivyokujanavyo mwanafunzi shuleni.

VIFAA VYA USAFI ANAVYOTAKIWA KUJA NAVYO MWANAFUNZI.

- Mchepuo wa **H G L,** Jembe 1 lenye mpini, dustbin 01 ya kati na soft broom 01
- Mchepuo wa **E G M**, Jembe 1 lenye mpini, dustbin 01 NA squeezer 01,
- Mchepuo wa **H G E,** Jembe 1 lenye mpini na spade (chepe 01)

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

I.Wizi.

II. Kutohudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 mfululizo bila taarifa

III. Kugoma na kuhamasisha mgomo.

IV. Kutoa lugha chafu (lugha ya matusi) kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

V.Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.

VI. Kushiriki au kufanya matendo ya uhalifu, na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za shule.

VII. Unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.

VIII. Uvutaji wa sigara.

IX. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja (ushoga na usagaji), kuoa au kuolewa.

X.Kupata ujauzito, kusababisha mimba, kutoa mimba.

XI.kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni (guest house)

XII. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

XIII. kudharau Bendera ya Taifa.

XIV.kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.n.k

XV. Uharibifu wa mali za shule kwa makusudi.

4. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU.

(a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.

(b) Passport nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni, namba zao za simu na anwani (sanduku la posta)

(c) Passport nne (04) za mwanafunzi akiwa amevalia shati jeupe

(d) Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

(e) Aje na result slip original ya kidato cha nne.

ZINGATIA

✓**Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

KARIBU SANA J.J. MUNGAI



NASHON.B. NDANZI
MKUU WA SHULE:



SHULE YA SEKONDARI J J MUNGAI
FOMU YA KUPIMWA AFYA.

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari J.J. Mungai,
S.L.P 226,
MAFINGA.

DAKTARI…….
HOSPITALI YA …….
S.L.P…….
……

YAH: KUPIMWA AFYA MWANAFUNZI

Tafadhali tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu kwa gharama za mzazi wake na uthibitishe kama ataweza kumudu masomo ya sekondari katika shule hii kwa vipengele vilivyoanishwa katika fomu hii:

JINA LA MWANAFUNZI…….

Matokeo ya vipimo vya afya ya mwanafunzi aliyetajwa hapo juu.

1. Urine ……...
2. Stool……...
3. H B ……...
4. Pregnancy Test……...
5. Spleen ……...
6. Chest …….
7. Limbs……...
8. Physical abnormality…….....

Nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu ……

Ataweza / hataweza kumudu masomo ya sekondari.

…… …… ……..
JINA LA DAKTARI SAHIHI CHEO

MUHIMU:

- ✓ **Kama mwanafunzi ana tatizo lingine la kiafya ni vyema mwanafunzi aje na cheti cha kitabibu.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIAOFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI MAFINGA
SHULE YA SEKONDARI J. J. MUNGAI

TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili……
2. Tarehe ya kuzaliwa…….. (tarehe, mwezi, mwaka)
3. Kabila ……. Uraia…….
4. Dini na dhehebu ……...
5. Jina la baba…… Uraia……
6. Anuani ya baba……...
7. Kazi ya baba …….
8. Jina la mama …….
9. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana……
10. Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea shuleni: -

S/N	JINA LA MZAZI/MLEZI	UHUSIANO	SIMU NA.	ANAKOISHI
1				
2				
3				
4				

PICHA 1	PICHA 2	PICHA 3	PICHA 4

11. Wakati wa likizo utakuwa kwa nani na wapi (taja sehemu moja tu utakayokwenda kila wakati na Anuani …….
12. Nathibitisha Kwamba habari zote nilizotoa hapa ni kweli na ni sahihi

Saini ya mwanafunzi…… Tarehe……

Saini ya mzazi/mlezi……. Tarehe……

ZINGATIA.

- ✓ **Wazazi na walezi wa mwanafunzi waweke passport zao kwenye vyumba vya picha kufuatana na mtiririko wa majina**

HALMASHAURI YA MJI MAFINGA.
SHULE YA SEKONDARI JJ. MUNGAI
FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

1. SEHEMU YA MWANAFUNZI

Mimi …… ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha tano katika shule ya sekondari JJ. Mungai na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kufuata sheria zote za nchi. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii kwenye masomo na kazi ya elimu ya kujitegemea. Nitakuwa mwaminifu na sitamiliki simu ya mkononi wala kushiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai kwa mda wote niwapo shuleni.

Anuani yangu ya kudumu ni

……

……

……....

2. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi……...
ninakubali mtoto wangu…….....
kujiunga na kidato cha tano katika shule ya J. J. Mungai 2022. Ninaahidi kumpatia mahitaji ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninaahidi kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na taifa na hatamiliki simu ya mkononi awapo shule wala kushiriki mgomo, fujo na makosa ya jinai kwa mda wote atakapokuwa mwanafunzi wa JJ. Mungai.

Anuani yangu ya kudumu ni

……...……...

……..……

……..

Simu Na. ……...

Iwapo nitapata uhamisho au kubadilisha makazi, ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi

Saini……tarehe……

OFISI YA RAIS TAMISEMI

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, NA MAFUNZO YA UFUNDI.

SHULE YA SEKONDARI J.J. MUNGAI

SHERIA ZA SHULE.

Mimi……kidato……...Mchepuo……

Ninakiri kuzifahamu na kuzifuata sheria na kanuni zote za shule kama zilivyoainishwa hapa chini.

A. HESHIMA:

1. Wanafunzi ni lazima wawaheshimu wafanyakazi wote shuleni kama walezi au wazazi wao.

2. Wanafunzi wanapaswa kusimama na kusalimu walimu, watumishi au watu wote waliowazidi umri mahali popote wanapokutana nao

3. Ni kosa kwa mwanafunzi kutumia lugha ya matusi

4. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mambo yafuatayo; -

(i) Kuvuta sigara.

(ii) Kufuga kucha ndefu, na kuwa na nywele ndefu.

(iii) Kufuga ndevu.

(iv) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima.

(v) Kugombana, kutumia lugha ya matusi.

5. Wanafunzi wanatakiwa kuitika mara moja na kukimbilia aliko mkuu anayewaita.

6. wanafunzi ni lazima kuheshimu Bendera ya Taifa, picha za viongozi, Nembo ya Taifa na Wimbo wa Taifa.

7. Wanafunzi wasimame kwa adabu wanapoulizwa maswali au wanapoongea na mtu aliyewazidi umri.

8. Hairuhusiwi kupiga kelele darasani, na pia kutoka nje ya darasa ila tu kwa ruhusa ya Mwalimu.

9. Wanafunzi wanapaswa kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote walipo.

B. MAHUDHURIO:

1. Ni lazima wanafunzi wahudhurie shule muda wote wa masomo.

2. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.

3. Kama mwanafunzi anatatizo lolote mfano ugonjwa, kama anataka kusafiri n.k sharti apate ruhusa maalum ya shule kupitia ofisi ya malezi.

4. Ni marufuku kuzurura nje wakati wa masomo.

C. KUWAHI:

1. Mwanafunzi ni lazima kukimbia kutoka sehemu **"A"** kwenda **"B"** na pindi itakapogongwa kengele ya wito.

2. Mwanafunzi wanapaswa kuheshimu na kuthamini muda.

3. Mwanafunzi anapaswa kuwahi katika shughuli za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku (DAILY ROUTINE).

4. Kila mwanafunzi analazimika kuheshimu kengele, na kutambua mara moja tukio litakalofuata baada ya kengele kugongwa.

D. SARE ZA SHULE:

1. Kila mwanafunzi lazima awe na sare ya shule kama ilivyoainishwa, ataivaa sare hiyo muda wote awapo shule kulingana na mazingira husika

2. Kila mwanafunzi ni lazima awe na nguo za michezo na viatu vya michezo.

3. Sare ya shule ni lazima iwe safi wakati wote inapovaliwa, mwanafunzi anatakiwa awe safi wakati wote.

4. Ni marufuku mwanafunzi kuvaa kofia au mzura na pia viatu virefu (HIGH HEELS) na MAPAMBO SHULENI.

5. Sare za shule ni lazima zishonwe kimaadili (sketi ndefu na suruali zisizobana)

E. MIPAKA YA SHULE:

1. Kila mwanafunzi ni lazima aielewe barabara mipaka ya Shule ambayo mwanafunzi ataelekezwa pindi atakapofika shuleni

2. Ni kosa kwa mwanafunzi kwenda nje ya mipaka ya Shule bila ruhusa ya uongozi wa shule.

3. Mwanafunzi anayetaka kwenda nje ya shule kama hospitali, dukani n.k sharti apate ruhusa kutoka kwa mwalimu wa zamu au mwalimu yeyote anayehusika. Pamoja na ofisi ya malezi.

4. Wanafunzi wasitembelee sehemu zifuatatzo isipokuwa kwa kibali cha mwalimu maalumu.

(i) CHUMBA CHA WALIMU (STAFF ROOM).

(ii) OFISI NYINGINE ZA SHULE.

(iii) MAABARA

(iv) JIKONI

(v) NYUMBA ZA WALIMU NA WAFANYAKAZI WASIO WALIMU.

5. Ni kosa kwa mwanafunzi kutembelea sehemu zifuatazo; -

(i) Vilabu vya pombe.

(ii) Majumba ya starehe.

(iii) Majumba ya kufikia wageni (GUEST HOUSE).

(iv) Nyumba walizopanga wanafunzi wa jinsia tofauti.

(v) Mahali pa michezo ya starehe i.e. Pool table na michezo ya kubahatisha

TANBIHI: KUTOZIELEWA SHERIA ZA SHULE NI KOSA KUBWA.



NASHON. B. NDANZI

MKUU WA SHULE